BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA FEDHA, BIASHARA NA KILIMO KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA BIASHARA NA VIWANDA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Mheshimiwa Spika,

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma kwa kutujaalia uzima na Afya njema tukaweza kukutana tena katika Baraza hili la Tisa kwa ajili ya kuendelea kuwatumikia wananchi wetu.

Nichukue fursa hii kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii adhimu na muhimu ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Viwanda kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Naomba pia

kukutakieni Ramadhani njema Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili tukufu pamoja na wananchi wote wa Zanzibar kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yetu inatoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda Balozi Amina Salum Ali kwa umahiri wake na umakini wa hali ya juu aliouonesha kila wakati kamati ilipokutana na Wizara hii. Shukurani za kipekee tunazitoa kwake kwa ushirikiano mkubwa aliotupatia katika kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Viwanda kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Vilevile, tunatoa shukrani za dhati kwa Naibu Waziri Mhe. Hassan Khamis Hafidh na watendaji wote wa Wizara hii kwa ushirikiano waliotupatia katika utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Kamati husuan katika kupitia bajeti ya Wizara ya Biashara na Viwanda.

Mheshimiwa Spika,

Tunatoa pongezi za dhati kwa Wizara ya Biashara na Viwanda kwa juhudi zake inazozichukua za kudhibiti bei za bidhaa muhimu za chakula kwa kuweka bei elekezi ambazo zinawapa unafuu wananchi hususan katika mwezi mtukufu wa Ramadhan bila ya kuwaathiri wafanyabiashara wa bidhaa hizo. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa bado kuna baadhi ya Wafanyabiashara ambao hawazifuati bei hizo kikamilifu na hivyo kuitumia fursa hiyo kujipatia faida kubwa zaidi. Katika uendelezaji wa shughuli hiyo muhimu, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inatoa wito kwa Wizara kufuatilia utekelezaji wa bei hizo sokoni ili kuwapa faraja wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika,

Shukurani za pekee nazitoa kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa ujasiri wao waliouonesha katika kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi

ya Wizara ya Biashara na Viwanda kwa mwaka 2018/2019 na hatimaye kuipitisha bajeti hiyo pamoja na marekebisho madogo madogo waliyoyafanya kwa nia ya kuimarisha zaidi utendaji wa Wizara. Kwa heshima kubwa napenda kuwatambulisha Wajumbe hao kwa majina kama hivi ifuatavyo:-

1. Mheshimiwa Yussuf Hassan Iddi - Mwenyekiti
2. Mheshimiwa Hamida Abdalla Issa - M/Mwenyekiti
3. Mheshimiwa Hamad Abdalla Rashid - Mjumbe
4. Mheshimiwa Moh'd Mgaza Jecha - Mjumbe
5. Mheshimiwa Ali Salum Haji - Mjumbe
6. Mheshimiwa Ussi Yahya Haji - Mjumbe
7. Mheshimiwa Bihindi Hamad Khamis - Mjumbe
8. Ndugu Asma Ali Kassim - Katibu
9. Ndugu Said Khamis Ramadhan - Katibu

Mheshimiwa Spika,

Jadweli la kwanza ambalo limeundwa chini ya Kanuni ya 106 ya kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la 2016, inazitaka Kamati za kisekta kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka. Katika utekelezaji wa matakwa ya kanuni hiyo, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilitekeleza wajibu wake kwa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Viwanda kwa mwaka wa fedha 2018/2019 mnamo tarehe 04/05/2018.

MheshimiwaSpika,

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Baraza la Wawakilishi ililiidhinishia Wizara ya Biashara na Viwanda Matumizi ya jumla ya Tshs. 4,460,200,000 kwa kazi za kawaida. Aidha, Wizara ililiidhinishiwa kutumia jumla ya Tshs. 2,750,000,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2018, Wizara iliingiziwa jumla ya Tsh. 4,080,910,000 ambazo ni sawa na

asilimia 56.6 ya makadirio ya mwaka. Vile vile, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara iliidhinishiwa kukusanya jumla ya Tshs. 455,224,000 kama ni mapato yatokanayo na vianzio mbali mbali katika Taasisi zake. Hadi kufikia Machi 2018, Wizara ilifanikiwa kukusanya jumla ya Tsh. 864,340,000 sawa na asilimia 190 ya makadirio ya makusanyo. Kamati yetu inatoa pongezi za dhati kwa Wizara ya Biashara na Viwanda kwa kuvuka lengo la makusanyo kwa mwaka 2017/2018.

PROGRAMU YA UKUZAJI NA UENDELEZAJI WA BIASHARA

Mheshimiwa Spika,

Kamati yetu imeshangazwa na kitendo cha kutotengwa fedha kwenye huduma ya (HR01030101) Uimarishaji wa Mazingira mazuri ya Biashara kwa mwaka wa fedha 2018/2019 jambo ambalo haliendi sambamba na sera ya Taifa ya kuelekea kwenye uchumi wa kati wa viwanda vidogo vidogo. Hivyo, Kamati inashauri kutengewa fedha huduma hii ili kuiwezesha Wizara

kuimarisha biashara nchini na kutanua wigo wa ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika,

(Kifungu 1146) Kodi nyenginezo kwa bidhaa na huduma kimepangiwa kuchangia jumla ya Tsh. 1,000,000 kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kamati yetu iliarifiwa kuwa kasma hiyo inahusisha mapato yatokanayo na mirathi ya wale wasiokua waislam ambayo itasimamiwa na Baraza la Usimamizi wa Usajili wa Biashara na Mali. Kimsingi, masuala hayo ya mirathi hayakupaswa kusimamiwa na Baraza hilo na hivyo, Kamati inashauri kasma hiyo ihamishiwe kwenye Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa vile shughuli za usajili wa vizazi na vifo ndiyo pahala pake.

Mheshimiwa Spika,

Hadi kufikia Machi 2018, Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) limekusanya malipo ya jumla ya Tsh. 280,000,000 ambazo ni sawa na asilimia 94 ya madeni ya wakulima waliokopeshwa kwa ajili ya kuliokoa zao la karafuu katika msimu uliopita. Kamati yetu inalipongeza Shirika hilo kwa juhudi zake za kuhakikisha fedha iliyotolewa na Serikali inarudishwa kwa ajili ya matumizi mengine. Ni imani yetu kuwa deni lililobakia la jumla ya Tsh. 8,000,000 litaendelea kulipwa kabla ya kumaliza mwaka huu wa fedha 2017/2018 na kutoa fursa kwa Serikali kuweza kuzitumia fedha hizo kwa shughuli nyengine za maendeleo.

PROGRAMU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRIAMALI

Mheshimiwa Spika,

Tukijikita katika suala zima la maendeleo ya viwanda nchini, programu ndogo ya ukuzaji viwanda (SR010201), imetengewa jumla ya Tsh. 3,665,290,000 kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Kiwango hicho ni kikubwa ikilinganishwa na fedha zilizotengwa kwa mwaka 2017/2018 ambazo ni Tsh. 644,987,000. Hata hivyo, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imebaini kuwa fedha hizo hazitoshelezi hata kuanzisha kiwanda kimoja na kwa msingi huo tunapendekeza programu ndogo hiyo iongezewe fedha zaidi kwa nia ya kuvianzisha, kuvilea na kuvilinda viwanda vyetu hadi kuviwezesha kuimarika na kuwa endelevu kwa manufaa yetu na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika,

Kushuka kwa fedha za huduma ya msaada kwa wajasiriamali (HR01020201) kutoka Tsh. 267,594,000 mwaka 2017/2018 hadi Tsh. 166,109,000 kwa mwaka 2018/2019 ni jambo lisilotarajiwa tukitilia maanani kwamba idadi ya Wajasiriamali wetu ni kubwa na wanahitaji msaada mkubwa ili kujikwamua kutoka katika dimbwi la umasikini. Hali hii inadhihirisha wazi kuwa bado hatujawa tayari kuelekea kwenye uchumi wa kati uliojengeka kwa

viwanda vidogo vidogo ambavyo ndio msingi wa ajira kwa vijana wetu na kuimarika kwa uchumi wetu. Hivyo, Kamati inapendekeza huduma hiyo itengewe fedha zaidi ili kufikia malengo tuliyojiwekea.

PROGRAMU YA VIWANGO NA TATHMINI YA UBORA.

Mheshimiwa Spika,

Ili kuimarisha pato la Taifa letu, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inashauri kusitishwa kwa mkataba baina ya kampuni ya Jabal Kilimanjaro ya Dubai na Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) inayohusiana na huduma ya ukaguzi wa magari yanayotaka kuingizwa nchini kutoka Dubai. Mkataba huo unaeleza kuwa asilimia 70 ya mapato ya shughuli hiyo yanaingia kwa Kampuni hiyo na asilimia 30 inarudi kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kiwango hicho kinachoingia nchini ni kidogo mno na hivyo Kamati inapendekeza mara baada ya kumalizika muda wa mkataba huo Serikali ivunje mkataba na kujipanga upya kwa

kuingia mkataba na Kampuni nyengine huko Dubai na kutafuta vifaa muhimu vya ukaguzi hapa Zanzibar ili kuzifanyia ukaguzi gari zilizokwepa kukaguliwa huko Dubai pamoja na kuweka kiwango stahiki cha faini ambacho watatozwa wale waliokwepa kukaguliwa. Aidha, Kamati inaiagiza Wizara kupitia ZBS kuwachukulia hatua kali wale wote wanaoingiza gari kwa njia ya kuzikata vipande vipande ili kukwepa ushuru na ukaguzi wa ubora wa magari hayo.

Mheshimiwa Spika,

Mwisho kabisa, napenda kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili Tukufu kwa umakini na usikivu wao wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii. Kwa vile Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Viwanda naomba Sasa nichukue fursa hii kuwakaribisha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kuichangia,

kuijadili, kuhoji na hatimaye kuipitisha bajeti ya Wizara ya Biashara na Viwanda kwa mwaka wa Fedha wa 2018/2019.

Mheshimiwa Spika,

Baada ya kusema hayo, Kwa niaba ya Mwenyekiti na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, naiunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Ahsante sana,

……..,

Hamida Abdalla Issa,
Makamo Mwenyekiti
Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo,
Baraza la Wawakilishi,
Zanzibar.